MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA

# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 27. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Juni 21-30, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Julai 01-10, 2018**

**Muhtasari**


- Vipindi vya hali ya ukavu vinavyo tarajiwa vitasaidia kukomaa kwa mazao pamoja na shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao.
- Uvamizi wa viwavi jeshi unahofiwa kuhatarisha usalama wa chakula katika maeneo yaliyoathirwa na wadudu hao.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita (dekadi) migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ili imarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) ulielekea kaskazini zaidi. Pamoja na kuimarika kwa mgandamizo mkubwa wa hewa wa kusini, kulikuwa na eneo lenye mgandamizo mdogo wa hewa hali iliyopelekea vipindi vya upepo mkali katika baadhi ya maeneo ya nchi. Joto la bahari katika maeneo ya kusini magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani na kusababisha kutokuwepo kwa vimbunga baharini.Upepo ulivuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi.Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kuliendelea kuwepo na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii ilisababibisha kupunguza kwa mifumo ya kusababisha mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, vipindi vifupi vya mvua za nje ya msimu zilinyesha katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususan maeneo ya nyanda za juu kaskazini pamoja na maeneo ya ziwa Victoria, ambayo yalipata mvua kati ya milimita 10 mpaka 100.Mvua za nje ya msimu pia zilionekana katika eneo magharibi mwa mkoa wa Morogoro ambapo kiasi cha milimita zaidi ya 500 kilipatikana kama inavyoonekana kwenye kielelezo chini.




**Kielelezo Na. 1**. Kiasi cha mvua kipindi cha tarehe 21-30, Juni, 2018.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2018

Katika kipindi cha dekadi iliyopita, wakulima waliendelea na shughuli za uvunaji wa mahindi katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, hususan katika mikoa ya Ruvuma, Mtwara, Rukwa na Njombe. Maeneo mengi yanayopata msimu mmoja wa mvua mahindi yalikuwa katika hatua ya kukomaa. Maharage yapo katika hatua ya kukomaa mkoani Mbeya, mpunga unavunwa katika mikoa ya Tabora na Kigoma.

Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua shughuli za mavuno zinaendelea, mpunga na viazi vinavunwa katika mkoa wa Shinyanga, maharage yanavunwa mikoa ya Mara na Kagera, na mtama unavunwa katika mkoa wa Mara. Mahindi yamearifiwa kuwa katika hatua ya kukomaa katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua. Mikoa ya Simiyu, Tabora, Shinyanga,, Mara na Kagera, wakulima wanaendelea na uvunaji wa mahindi. Hali ya maji na malisho kwa ajili ya wanyama ilikuwa ya kuridhisha isipokuwa mikoa ya Dodoma na Tabora ambapo maji yameanza kupungua

Uharibifu uliotokana na mafuriko - mvua za masika pamoja na viwavi jeshi vimeathiri mazao kwa kiasi kikubwa na kusababisha uhaba wa chakula hususan katika maeneo ya Mwanga (wilaya ya Same), ambapo wakulima wanapata msaada wa chakula kutoka serikalini.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA JUNI 21-30, 2018

Kina cha maji katika mabwawa, mabonde na mtiririko wa maji katika mito ilikuwa ya wastani, isipokuwa bonde la ziwa Victoria na Pangani ambapo hali ya maji inaonesha kuwa nzuri zaidi.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 01-10, 2018

Katika kipindi hiki, Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azorena Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuendelea kusogea kuelekea kaskazini hali itakayopelekea upepo kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki katika maeneo mengi ya nchi. Joto la bahari lawastani hadi chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hali itakayoondoa uwezekano wa kutokea vimbunga katika bahari. Upepo unatarajiwa kuvuma kutoka kusini hadi kusini mashariki hali itakayopekekea hali ya baridi katika maeneo mengi ya nchi. Eneo la Kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi juu kidogo ya wastani. Hali hii itapelekea kupunguza kwa upepo uvumao kutoka magharibi hivyo kupunguza nguvu ya mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 01-10,2018

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zinazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) na Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) inatarajiwa kuwa na mvua nyepesi katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) inatarajiwa kuwa na mawingu kiasi.

Nyanda za juu Kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro) inatarajiwa kuwa na mawingu kiasi kwa ujumla.

## MATARAJIO NA USHAURI WA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 01-10, 2018

Hali ya ukavu inayotarajiwa itasaidia kukomaa kwa mazao pamoja na shughuli za uvunaji na uhifadhi wa mazao. Wakulima wanashauriwa kuweka akiba ya ziada ya chakula na kukitumia kwa uangalifu kuepuka janga la njaa, hususan katika maeneo yaliyoathiriwa zaidi na viwavi jeshi.

Hali ya maji pamoja na malisho vinatarajiwa kuwa katika hali nzuri na inayotosheleza katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maofisa ugani kwa ajili ya kupata ushauri na matumizi sahihi ya utabiri huu.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 01-10,2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuwa vya wastani katika sehemu nying nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji kwa uangalifu kwa matumizi endelevu ya rasilimali hii.

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:***